

MUNGU ASIYEBADILIKA



...muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

² Baba yetu wa Mbinguni, ni majaliwa makuu tuliyo nayo ya kuja katika Uwepo Wako katika mtazamo huu wa ibada na sifa Kwako, na kujua ya kwamba tunaweza kukuita Baba yetu. Kwa kuwa tumezaliwa na Roho Wako, sisi ni watoto Wako, na tukiwa na majaliwa ya kuomba tutakacho, nayo imani itatuletea. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

³ Mungu Mtakatifu sana na Mwenye Haki, tungeomba, usiku wa leo, ya kwamba ungesema na wale, Bwana, walio wahitaji, wale wanaohitaji wokovu wa nafsi zao, na kwa wale walio wagonjwa na walio katika hali ya kukata tamaa, kwa waliofungiwa, wale walio hospitalini na wamelazwa hospitalini, wala hawawezi kufika mkutanoni, Ewe MIMI NIKO aliye MKUU, nenda kando ya vitanda vyao, usiku wa leo, na uiguse miili yao migonjwa, ili waweze kutoka hospitalini kukutumikia Wewe.

⁴ Tusamehe dhambi zetu kama tunavyowasamehe wale wanaotukosea, ili tuweze kuwa na kibali Chako miongoni mwetu usiku wa leo. Na useme nasi kupitia Neno Lako. Neno Lako ndilo Kweli, lifanye lijulikane kwetu, Bwana, lifanye Neno Lako liishi miongoni mwetu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mtoto Wako, Bwana Yesu. Amina.

⁵ Mwaweza kuketi. Sasa, kwa ajili ya kuendeleza tu ujumbe, hakika nilichukuliwa sana, na kusimama pale nikimsikiliza Ndugu du Plessis akileta ujumbe huo juu ya Mtume Petro kuweza kutembea juu ya maji, jambo ambalo hakuwahi kufanya hapo awali. Nasi tunaweza tu kufanya mambo mengi ambayo hatujawahi kufanya hapo awali kama tu tutasikiliza Neno Lake, na kuamini Neno Lake kwa ajili yake. Yeye kamwe hakutoa ahadi asiyoweza kuunga mkono.

⁶ Sasa, ibada inaanza Jumapili saa ngapi, ndugu, Jumapili? Saa nane na nusu. Vema, hiyo inamaanisha yapata saa saba na nusu wale wanaotaka kadi za maombi wanapaswa kuwa hapa saa saba na nusu basi, kusudi msisumbue mikutano wakati wanapogawa kadi za maombi. Na kwenye saa nane na nusu ibada zinaanza, ndipo tutatoka katika wakati mzuri kwenu kwenda nyumbani na kula ninii chenu... Je, ni chakula cha kutwa au cha jioni hapa? Mimi ni mkusini, na ni—ni chakula cha jioni kwangu. Kama wakiita hicho chakula cha kutwa, basi ilikuwaje kwa chakula changu cha jioni? Nimekosa mahali fulani. Kwa hiyo mimi—mimi...Mwende nyumbani kwa chakula chenu cha jioni, hivyo ndivyo ningekiita. Halafu mwende kwenye... makanisa yenu. Nao wageni malangoni petu,

tunataka, mnaotembelea hapa, makanisa haya mazuri yatakuwa na shule ya Jumapili, Jumapili asubuhi na kanisa, Jumapili usiku, jitafutie mahali pa chaguo lako uhudhurie ibada hiyo.

⁷ Na, sasa, kwa namna fulani ninafurahia mkutano huu kwa sababu nyingi, kwa sababu nimeutazamia kwa muda fulani nipate kurudi.

⁸ Ningependa kunukuu tu kifungu kimoja kutoka katika Kitabu cha Ayubu usiku wa leo, mlango wa 23 na kifungu cha 3:

Laiti ningalijua mahali niwezapo kumwona! nifike hata hapo anapokaa!

⁹ Hicho ni Ayubu 23:3. Nitazungumza kwa dakika chache juu ya somo la *Mungu Asiyebadilika*, kama ningeliita somo.

¹⁰ Kuna vitu vingi, na karibu vitu vyote hubadilika. Wakati hubadilika, watu hubadilika, hali ya hewa hubadilika, mataifa hubadilika, bali Mungu habadiliki, Yeye habadiliki, Yeye ni yeye yule nyakati zote.

¹¹ Mungu ni Mungu asiye na kikomo. Siamini ya kwamba kungekuwa na neno lolote lingeweza kuelezea hilo—hilo neno, ama, njia yoyote ya kuelezea neno *pasipo na kikomo*, kwa sababu ni kutokuwa na kikomo. Hajawahi kuwa na mwanzo, wala hatakuwa na mwisho kamwe, kwa hiyo wakati Mungu anapoitwa jukwaani kutenda kazi, ama kufanya uamuzi, jinsi anavyotenda, ama uamuzi anaofaya, huo ni ule ule milele. Hawezi kuubadilisha, kwa sababu Yeye hana kikomo, Yeye ni mkamilifu.

¹² Sasa, mimi na wewe tunaweza kusema jambo fulani, na mwaka ujao itatubidi kulibadilisha, labda, na kufanya jambo tofauti, ama, kwa sababu tuna kikomo, ha—hatujui mambo yote. Lakini Yeye ni mkamilifu, na uamuzi Wake wa kwanza itabidi uwe... Uamuzi Wake wa pili, itabidi uwe kama ule wa kwanza, la sivyo, kama akifanya uamuzi mwingine, basi hakufanya vizuri wakati alipofanya uamuzi wa kwanza, basi hilo linamfanya Yeye kuwa na kikomo kama nilivyo mimi au ulivyo wewe.

¹³ Ninachojaribu kufanya, kabla ya ibada hii ya uponyaji kuja, ni kuingiza ndani yenu imani katika Mungu, kwa sababu hiyo ndiyo inayohitajika kwa uponyaji ama wokovu. Lazima umwamini Mungu, na Mungu si mkuu kuliko Neno Lake, au si mkamilifu kuliko Neno Lake, kwa sababu Mungu na Neno Lake ni kitu kile kile. Wewe si—si bora kuliko neno lako; Mungu si bora kuliko Neno Lake. Na neno lako ndivyo ulivyo; Neno la Mungu ndicho kile alicheo Yeye.

¹⁴ Sasa, mtu yeyote anajua ya kwamba kama Mungu aliitwa jukwaani wakati mmoja, kumwokoa mtu aliyepotea, halafu Mungu akamwokoa mtu huyo kwa imani yake, mtu mwingine anayemwita Mungu, itambidi Mungu kumwokoa mtu huyo kama akija kwenye misingi ile ile ambayo mtu wa kwanza alikuja.

¹⁵ Basi kama kuna mtu mgonjwa naye anamsihi Mungu amrehemu, halafu Mungu ampe rehema na uponyaji juu ya msingi wa imani yake, mtu mwingine anayekuja kwenye misingi ile ile, na kuuliza swali lile lile, Mungu hana budi kutenda vivyo hivyo, la sivyo alikosea wakati alipotenda mara ya kwanza. Kwa hiyo mnaona, hatuna budi kumfanya Mungu halisi, asiyeabadilika.

¹⁶ Kila mtu amjiaye Mungu akitafuta wokovu ama uponyaji, hana budi kuja kwa misingi hiyo. Hana budi kuja akiamini ya kwamba Mungu yupo, na Mpaji thawabu wale wamtafutao kwa bidii.

¹⁷ Hivi Bwana wetu Yesu hakusema, “Yoyote mtakayo, mkiomba, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu”? Hivi Yeye hakusema, “Mwombeni Baba mtakalo katika Jina Langu, nanyi mtayapokea”? Sasa, huo ni ukweli usioweza kukosea. Wala hakuna mtu aliyewahi kumwomba Mungu chochote, ila ambaye Mungu alimpa kama wakija na moyo mnyofu.

¹⁸ Sasa, jambo ni kwamba, Mungu wakati mwingine hutupa kwa njia ambayo hatuitarajii, bali Mungu daima hulitimiza Neno Lake. Hakuna njia kwa Mungu kukwambia lolote na kusema uwongo juu yake na abaki Mungu. Hawezi, hana budi kulisitiza Neno Lake milele, ni kweli. Na wakati Biblia inaposema ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hiyo ni kweli.

¹⁹ Huenda nisiwe na imani ya kutosha kuyafanya mambo yote aliyofanya, yaishi tena, bali kamwe nisingesimama katika njia ya mtu aliyekuwa na imani ya kutosha kuyafanya. Ningekuwa nikimshukuru Mungu kwa ajili ya imani hiyo. Lakini vile vile tu, kila ahadi aliyotoa ni kweli kabisa.

²⁰ Ninaweza kuingia kwenye kumbukumbu kwa ajili ya hili usiku wa leo: Ikiwa watu wowote watachukua mtazamo sahihi wa kiakili kuelekea ahadi yoyote ya Kiungu ambayo Mungu aliwahi kuitoa na kuidai kuwa ni yenu, Yeye ataninii, Mungu ataifanya kutimia. Kama utachukua mtazamo mzuri juu yake, ukijua ya kwamba kama Mungu alisema hivyo, hiyo ahadi ni yako, na ni mali yako binafsi dakika ile ile unapoipokea hivyo, basi haina budi kutimia.

²¹ Kwa kuwa Yesu alisema, “Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda.” Nayo mbegu, kama ni mbegu iliyorutubishwa na ingie ardhini, basi mbegu hiyo chini ya hali nzuri ya jua na unyevu, itazaa uhai ulio ndani ya hiyo mbegu.

²² Na vivyo hivyo na Neno la Mungu. Kama mtu anaweza kuchukua Neno hilo na kuliweka moyoni mwake, na kulipa Mwangaza mzuri wa Mwana, joto linalofaa, si j-u-a, lakini M-w-a-n-a, na joto la kutosha la imani humo ndani, hiyo Mbegu na ahadi itaishi kwako, kama tu ilivyofanya hapo mwanzo kwa

yule aliyepewa hiyo. Kwa sababu ni Neno la Mungu, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele; hawezi kushindwa.

²³ Sasa, jambo hilo liko kwa watu, ni jinsi Mungu anavyoonekana. Mara nyingi tunataka kufanya sanamu kutoka kwa Mungu, tunamwomba Mungu afanye jambo fulani, halafu ati hana budi kulifanya jinsi tu tuombavyo, la sivyo tutasema kamwe hakujibu. Tunapofanya hivyo, tunadhoofisha imani yetu katika Mungu; na tunadhoofisha ushuhuda wetu tusipoliamini Neno Lake.

²⁴ Mungu daima hujibu. Hakuna mtu aliyewahi kuuliza... Yesu alisema, “Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata. Kila mtu aombaye atapewa; kila atafutaye atapata; kila abishaye, atafunguliwa.”

²⁵ Sasa, hiyo ndiyo njia pekee, ambayo daima nimeipata, ambayo ninaweza kupata chochote kutoka kwa Mungu, ni kulihamini Neno Lake na kulihamini jinsi anavyolituma.

²⁶ Sasa, kama hatulichukui jinsi tu tunavyowazia ndivyo lilivyo, tumemjenga Mungu kama sanamu. Hana budi kujibu kulingana tu na njia zetu, la sivyo, “Vema, haifai kitu, Yeye hakutujibu.” Mungu hujibu kwa njia nyingi, Yeye hujibu kwa njia za kipekee, nyakati, na kila kitu ni cha kipekee.

²⁷ Tutachukua, kwa mfano, Musa. Musa alikuwa na umri wa miaka themanini, alikuwa karibu, unaweza kuwazia, ni mzee sana Mungu asiweze kuhusika naye. Alikuwa ni mzee, ambaye hakutarajiwa katika umri wake kushughulikiwa, na Mungu; jambo lingine, alikuwa chini ya Mlima Horebu, mahali pasipotarajiwa. Mungu alikutana naye katika umri usiotarajiwa, mahali pasipotarajiwa, katika njia isiyotarajiwa. Mungu hakukutana na Musa jinsi alivyokutana na wanadamu kwa kawaida, alikutana na Musa katika njia isiyo ya kawaida, katika njia aliyochagua kukutana na Musa.

²⁸ Hivyo ndivyo anavyoyajibu maombi yetu, kwa njia anayowazia ni bora kuliko zote. Na njia Yake daima ni sahihi. Kama tukiomba jambo lolote, nalo lisitendeke jinsi tu Mungu, ama, jinsi tunavyowazia kwamba Mungu anapaswa kuliacha litendeke, basi hilo linatufanya tushindwe na kurudi nyuma. Hebu na tumwomba Mungu, tusimame imara juu ya Neno, na kusema ni kweli, na kulipokea tu jinsi Yeye anavyolituma. Hivyo ndivyo inavyokupasa kumwamini Mungu.

²⁹ Huenda likaja limejificha, linaweza kuja kwa njia nyingine, njia ya mzunguko, lakini haidhuru inakuja kwa njia gani, kama tumeomba tutapokea, Mungu alisema hivyo. Na hilo latosha milele kama Mungu akisema hivyo, sasa, unapoanza kumchukua Mungu namna hiyo na kulihamini.

³⁰ Sasa, Musa, vipi kama angekuwa amesema, “Nilimwomba Mungu anifanye mwanajeshi, Naye huyu hapa katika kichaka

kinachowaka moto”? Haileti tofauti yoyote jinsi Mungu alivyomtokea, mradi tu alitokea.

³¹ Hilo tu ndilo muhimu hapa, maadamu Mungu anakuja na kujibu, maadamu tunatambua kuwa ni Mungu.

³² Yakobo, mtu mwingine, alishikwa kati ya nyakati mbili. Alikuwa amefanya mambo maovu, maskini hila kadhaa za kijanja kwa m—mkwewe, Labani. Naye alikuwa akimtoroka baba mkwe wake, akirudi nyumbani kwa mama. Ndipo alipokuja kujua, huyu hapa ndugu yake anakuja ambaye alikuwa amemfanyia hila chafu, ujanja mdogo, alikuwa yuaja, akikutana naye na jeshi.

³³ Kumbuka tu, dhambi zako zitakupata. Ndipo basi Yakobo, akiwa amefadhaika sana, na amechanganyikiwa, na katika shida, aliwapanga wake zake kuvuka kile kijito kidogo, akarudi upande ule mwingine mahali pasipotarajiwa, na wakati usiotarajiwa, akakutana na Mungu kwa njia isiyotarajiwa. Ni njia ya jinsi gani ya kukutana na Mungu! Katika mashindano ya mwereka, bali ilikuwa ni Mungu. Haidhuru kama Yeye yuko kwenye kichaka kilichowaka moto ama kwenye mashindano ya mwereka, ilikuwa ni Mungu.

³⁴ Na jambo muhimu lilikuwa, kwamba Yakobo, alikuwa ameota ndoto, na maono, na kadhalika, lakini huu ulikuwa ni wakati mmoja ambapo angeweza kuweka mkono wake juu ya Kitu fulani na kusema ni Mungu. Naye aliweza kukishikilia mpaka baraka ikaja.

³⁵ Loo, laiti tungeweza kufanya hivyo, kama tungeweza kupata mahali ambapo tungeweza kumwona Mungu, kama ni katika Neno Lake, popote pale, na kutambua kwamba ni Mungu, na kushikilia mpaka baraka ije! Ipiganie mwereka na Mungu. Mungu aliahidi kufanya hivyo. Mungu alisema kama tungetafuta, tungepata; ombeni, nanyi mtapewa; bisheni, mtafunguliwa. Kila Neno ni kweli.

³⁶ Wakati Yakobo aliposhika Kitu ambacho angeweza kukiangalia, akakishika kwa mikono yake, na kuona ya kwamba ilikuwa ni Mungu, asingekiachilia.

³⁷ Loo, laiti Ukristo ungeweza kufanya hivyo! Kama unaweza kuweka mkono wako ushike kitu ambacho ni halisi, upate ono la Mungu na kuona Uwepo Wake, na ukishikilie, mpaka Mungu atakaporudisha jibu na baraka, ni uamsho wa jinsi gani ungetokea hapa Tulsa, kama watu wangeweza kufanya hivyo, wangeweza kuona nguvu za Mungu aliye hai, kitu halisi. Haidhuru kinakuja katika hali gani, tuna mawazo yetu, bali Mungu ana njia ya kututumia vitu, kujibu maombi yetu.

³⁸ Kumekuwako na mikutano ya maombi inayoendelea hapa katika jiji hili kwa muda mrefu, kwa ajili ya uamsho, ninaamini, kama tungefungua tu macho yetu na kuwa tayari kuupokea, Mungu angeutuma kwetu kwa njia Yake ya kufanya hivyo,

katika wakati Wake Mungu angejalia jambo hilo. Lakini hatuna budi kutambua tumeomba, na kama tuliomba, basi tutapokea.

³⁹ Naye aliishikilia. Wakati usiotarajiwa, mahali pasipotarajiwa, na njia isiyotarajiwa, lakini alipotambua ya kwamba ilikuwa ni Mungu, aliishikilia.

⁴⁰ Isaya, yule nabii kijana, alikuwa amekuwa na maisha mazuri sana, alikuwa ameegemea kwenye mkono wa mfalme huyo mzuri, na kila kitu kikatokea vizuri, naye alikuwa na mafuta na ni mnene kupita kiasi kutokana na kula. Basi siku moja huyo mfalme akafa, naye Isaya akaingia katika ono. Alipoona pindo za Bwana, aliwaona Malaika wakiruka kupitia jengoni, wakiwa na mabawa juu ya uso wao, na mabawa juu ya miguu yao, na kuruka kwa mabawa mawili, wakilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!”

⁴¹ Naye alipoona jambo hilo, na kujua ya kwamba alikuwa amesimama katika Uwepo wa Mungu Mtakatifu, alisema, “Ole wangu! Kwa kuwa mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na ninaishi miongoni mwa watu wachafu.”

⁴² Naye Bwana alikuwa analia, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?”

⁴³ Ndipo yule Malaika akachukua makoleo na kuchukua makaa kutoka madhabahuni na kuyagusisha kinywani mwake na kumtakasa. Ilikuwa ni tamasha isiyo ya kawaida kwa huyo nabii, ilikuwa ni njia isiyo ya kawaida ambayo Mungu alihusika naye. Lakini Mungu anajua jinsi ya kuhusika na mwanadamu.

⁴⁴ Isaya alikuwa amelimishwa, na—na shuleni pamoja na mfalme, na kadhalika, alikuwa na kilicho bora zaidi ambacho angeweza kumpa kiakili, nadhani, katika akili zake. Lakini ilimbidi Mungu kumfanya nabii kwa kujifunua Mwenyewe kwake, kwa kumpa kitu halisi, ambacho angeweza kuona hakikuwa zaidi katika fasihi, na kusoma, na kuandika, bali mambo aliyokuwa amesoma kumhusu Mungu na kusikia kumhusu Mungu, yalidhihirishwa moja kwa moja mbele zake.

⁴⁵ Ndipo akasema, “Mimi ni mwenye midomo michafu, na ninashughulika na kukaa miongoni mwa watu wachafu.” Ndipo Mungu akamwandaa kwa ajili ya siku zake za unabii. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo mambo, Yeye huyafanya kwa njia isiyoeleweka.

⁴⁶ Nabii Eliya, tunaweza kumwazia kwa muda kidogo. Huyo hapo, amelala huko nyuma pangoni, alikuwa ameona nguvu za Mungu siku chache kabla ya hapo, siku arobaini hapo kabla. Alikuwa na nguvu za Mungu, alikuwa ameomba, na miaka mitatu na miezi sita haikuwa imenyeshwa. Ndipo akaomba tena juu ya mlima, na Moto ukashuka kutoka Mbinguni na kuiteketeza hiyo dhabihu, kisha akaomba tena, na mvua ikaja na kuiosha dunia. Halafu basi, kwa hofu ya tishio la

malkia, alikimbilia nyikani, alijua alikuwa amekosa kitu fulani, kulikuwa na kitu ndani yake ambacho hakikuwa sawa bado.

⁴⁷ Aliporudi ndani ya pango, kukaja tetemeko la ardhi huko nje ambalo lilitikisa pango alimokuwa ameketi. Kukaja upepo wenye nguvu ukienda kasi, kukaja ngurumo, na radi, na uvumi, na yote yalikuwa ni Mungu, bali hayakumvutia huyo nabii, hayakumgusa, kwa namna fulani.

⁴⁸ Alijua nguvu za Mungu zilikuwa nini, alijua Mungu alikuwa ameitikisa milima, na alikuwa na pepo zikienda kasi, na kadhalika, na kutuma Moto kutoka Mbinguni. Lakini alingojea, ndipo chini kabisa ndani yake ikaja Sauti ndogo, tulivu, iliyomvutia huyo nabii. Kulikuwa na kitu fulani, alikuwa ameona nguvu Zake za kufanya mambo, lakini wakati huu alihisi Uwepo Wake, na Sauti ndogo tulivu ikinena ndani ya moyo wake. Ndipo nabii akasimama akaenda hata mwisho wa hilo pango.

⁴⁹ Wakati mwingine tunaomba mambo, tunapata kitu vinginevyo. Tunamfanya Mungu kitu ambacho tunataka kumfanya ajibu jinsi tunavyodhani anapaswa kujibu.

⁵⁰ Israeli, kuna kisa kingine, Israeli ilikuwa ikimtaamia Mfalme mwenye nguvu kuja kuwapiga Warumi kwa fimbo ya chuma. Mungu aliwapa nini? Mtoto mchanga. Badala ya Mfalme mwenye nguvu, Yeye aliwapa Mtoto mchanga aliyevikwa nguo za kitoto, kasema, “Mtamwona amelala horini.”

⁵¹ Hakuja jinsi walivyomtarajia kuja, nao wakamkataa. “Haina budi kuja kwa njia yetu la sivyo haifai kitu.” Wakasema, “Mrudishe.” Naye akafanya hivyo. Hiyo ni kweli. Huna budi kuipokea jinsi Mungu anavyoituma, na kuifurahia.

⁵² Mungu hutia nanga kitu fulani kidogo moyoni mwako, na kusema, “Hiki ndicho.” Kiamini, kishikilie. Hilo ni Neno la Mungu, Yeye ameahidi atalithibitisha kwako, na kama akilithibitisha Neno, lishikilie.

⁵³ Naam, hawakumtaka Mtoto huyo. “Kama huwezi kututumia Mfalme, mbona, hatumtaki huyo mtoto mchanga, unaweza tu kumrudisha.” Angalieni haina budi kuwa ni njia ambayo—ambayo tunafikiri inapaswa kuwa.

⁵⁴ Hatuna budi kukumbuka ya kwamba Mungu hulifanya kwa njia Yake. Nayo njia Yake daima ndiyo njia sahihi. Hatuna budi kuamini yale Mungu aliyosema kulihusu, na kujua ya kwamba ni kweli kabisa, na kudumu nalo, kulishikilia.

⁵⁵ Yesu, alipofanyika Mwanadamu, alikuwa mnyenyekevu. Basi Mfalme wa—wa Mbingu angewezaje kuwa na mate usoni Mwake, na kitambaa kichwani Mwake, na kumpiga kwa fimbo? Kisha kasema, “Aisee, wananiambia wewe ni nabii. Tuambie ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini,” wala kamwe hakufungua kinywa Chake. Hilo lingewezekanaje?

⁵⁶ Mfalme waliyekuwa wakimtaamia, alikuwa anaenda kuupiga ulimwengu. Lakini Mungu aliwatumia Mfalme, na kwa sababu Mungu alimtuma katika njia Yake, basi walikataa kuliadini. Lakini Mungu alikuwa na njia hiyo ya kufanya kumtuma, wala hakumtuma kwa njia nyingine yoyote ila ile Neno Lake lilisema angekuja. Lakini walikuwa wamekata kauli ilibidi iwe kwa njia nyingine. Hapo ndipo tunapokosea, enyi marafiki, hapo ndipo shida ilipo.

⁵⁷ Wakati yule mtangulizi Yohana Mbatizaji alipokuja, sauti ya mtu aliaye nyikani, mbona, Biblia ilisema, “Mahali pote palipoinuka patashushwa, na mabonde yote yatainuliwa,” na mambo haya yote yangetukia, milima ingeruka kama kondoo dume wadogo, na majani yangepiga makofi yao. Mbona walikuwa wanatarajia mtikiso wa mtu huyu akishuka kutoka kwenye ushoroba wa Mbinguni, kabisa amevikwa kitani nzuri, na taji kichwani mwake, ama chochote kile.

⁵⁸ Nini kilitukia? Mungu aliwatumia maskini mhubiri huko nyikani huku amejifunga kipande cha ngozi ya kondoo, alionekana kama mdudu aliyejaa manyoya, uso wake umejaa mandevu. “Loo, mwondoeni jamaa kama huyo, akila nzige na asali ya mwituni. Hatutaki uhusiano wowote na kitu hicho. Huyo angeweza kumtangulia Masihi?” Lakini ilikuwa ni njia ya Mungu ya kumtangulia Masihi.

⁵⁹ Hatuna budi kulipokea kwa njia ambayo Mungu alisema, Mungu anapendezwa nalo, hiyo ndiyo njia Yake. Yeye ni hekima yote, Yeye ana nguvu zote, Yeye ni mwenye nguvu zote, yuko kila mahali, loo, Yeye ni Mungu, yule MIMI NIKO. Sio “nilikuwa,” ama “nitakuwa.” Lakini “MIMI NIKO, yeye yule milele.” Yeye ni Mungu, Naye hufanya mambo kwa njia za siri. Na, bali Yeye hufanya hivyo kwa ajili ya utukufu Wake Mwenyewe. Anafanya hivyo kwa sababu ni bora zaidi kulifanya hivyo. Hatuna budi kulipokea jinsi Yeye anavyolituma.

⁶⁰ Nina hakika ya kwamba chati zetu zote na kalenda, na kadhalika, ambazo tumezichora, Yesu akiya juu ya wingu, huyo mwingine amemchora amepanda farasi mweupe, na yote namna hiyo, itakuwa tofauti kabisa atakapokuja. Haitakuwa jinsi tulivyopanga, na wengi watakosa kuiona.

⁶¹ Wengi watashindwa kuiona siku hii tunayoishi. Wengi wanakosa kuona ishara ya kuja kwa Masihi, sasa hivi. Watu wengi wanashindwa kuiona, wao—wao, liko papo hapo mbele zao, hata hivyo wao—wao hawalioni.

⁶² Yesu alisema, aliponena katika—katika Luka, naamini ndipo, Naye akasema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Mliona jinsi alivyosema maadili ya watu katika siku za Nuhu? “Wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.” Lakini aliposema, “Sodoma,” aliiacha

tu, huo ulikuwa ni Moto ulioitekeza Sodoma. Moto ndio unaoshika dunia siku hizi. Hebu tulipitie hilo kwa dakika chache.

⁶³ Ibrahimu, akiketi huko nje, bila kutarajia chochote, alikuwa katika nchi yenye ukame kuliko zote, ilikuwa kwenye joto la mchana, wakati usio wa kawaida kwa jambo fulani kutukia, bali alimwona Mtu akija kwa miguu, watu watatu. Kitu fulani moyoni mwake kikamwambia ilikuwa ni Mungu, naye akashikilia. Asingewaruhusu wapite. Ee Mungu, jalia hilo litendeke hapa! Usiliache lipite, lishikilie.

⁶⁴ “Karibu ndani, keti chini ya mwaloni. Nitachota maji kidogo, nitakuwa mtumishi Wako, jalia niioshe miguu Yako. Nitakuletea kipande cha mkate, uishibishe nafsi Yako, ndipo waweza kuendelea. Kwa sababu hii Bwana wangu amekuja kwangu.” Hata hivyo, hakuwa na hakika sana, bali alijua ya kwamba kulikuwa na kitu kilichowaka moyoni mwake, “Hapana shaka wakati umewadia.”

⁶⁵ Wakati Mtu huyo alipoketi na kuzungumza naye, angalia kile alichofanya, aliangalia chini, akasema, “Ibrahimu,” Mgeni, alijua jina lake lilikuwa Ibrahimu? “Yu wapi Sara, mkeo?” Alijua alikuwa na mke, na alijua jina lake lilikuwa Sara.

Nayo Biblia ilisema ya kwamba Ibrahimu alimwambia, “Hemani nyuma Yako.”

⁶⁶ Naye akasema, “Mnaona, kwamba Ibrahimu ndiye mrithi wa ulimwengu, je, nimfiche Ibrahimu chochote, kwa kuwa yeye ni mrithi wa ulimwengu?” Naye akasema, “Katika muhula wake, nitakuzuru.”

⁶⁷ Naye Sara, mwenye umri wa miaka tisini, huko nyuma hemani nyuma Yake, kamwe hakumwona, kamwe hakujuu lolote kumhusu Yeye, wala Yeye hakujuu habari za Sara, naye akacheka moyoni mwake, labda namna *hiyo*, akaweka mikono yake kinywani mwake.

⁶⁸ Naye Malaika huyu, huku amegeuza mgongo Wake, akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Huyu alikuwa ni nani? Hakutarajia kabisa Mtu huyo kuwa Yule aliyekuwa. Lakini alipoanza kuondoka, Ibrahimu alimwita Elohimu, Mungu Mwenyezi.

⁶⁹ Ilikuwa ni ishara ya nini? Kwamba Mungu Mwenyezi, katika umbo la Roho Mtakatifu katika siku za mwisho kabla ya ulimwengu huu kutekelezwa, atakuja kwa watu Wake na kuishi miongoni mwa watu Wake katika mwili, akijitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa Lake kabla tu ya ule Moto kushuka. Kabla tu ya maangamizi ya ulimwengu, Elohimu, Mungu, Roho Mtakatifu ataingia miongoni mwa watu Wake na kufanya ishara alizofanya wakati huo. Loo, Yeye ni Mungu asiyebadilika.

⁷⁰ Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi, hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wasamaria, vivyo hivyo. Wengi wa kanisa walimwamini: “Loo, yeye ni Beelzebuli.” Lakini wale walioiona, na kuitambua kuwa ni Mungu, walitambua kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

⁷¹ Wale wanawake kisimani, alisema, “Bwana, Masihi yuaja, tunajua ya kwamba Yeye atatuambia mambo haya. Huna budi kuwa nabii Wake.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

⁷² Akakimbia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu!” Bila kutarajiwa angempata Mtu kama huyo. Jambo lisilotarajiwa lilikuwa ni kumwona Masihi duniani, akiishi miongoni mwa watu Wake.

⁷³ Ndivyo ilivyo siku hizi, watu hawatarajii, wanatarajia kitu kingine, wanatarajia mabomu, na kadhalika, kuanguka, ambayo labda yataanguka, wanatarajia muungano mkubwa miongoni mwa watu wa kanisa. Sasa huenda ikawa, lakini katikati ya hayo yote, Mungu ametuma nguvu za Mwanawe, Yesu Kristo, miongoni mwa watu, nao wanakuwa na Pentekoste mpya, nguvu za Mungu zikimwagwa, na ishara zile zile na maajabu waliyofanya miaka mingi iliyopita yako katikati ya watu, kama Yesu alivyosema yangekuwa. Hatutarajii muungano miongoni mwa makanisa yote na kadhalika, tunatazamia kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, Naye atakuja na kufanya mambo ambayo, ambayo huenda hatuyatarajii.

⁷⁴ Ninajua Yeye yupo hapa sasa, ninajua Roho Mtakatifu yuko hapa mkutanoni, nami ninajua ya kwamba Yeye aliahidi, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika ninii Yangu...katika ninii yao...pamoja, nitakuwa katikati yao.” Yesu aliahidi ya kwamba, “Walipo wawili au watatu,” hizo ndizo nguvu, hicho ndicho, kile Kanisa la mwanzoni lilichotegemea, Uwepo wa Yesu, “walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Na lolote watakalokubaliana, kuhusu jambo moja, na kuomba, watalipokea.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni ahadi ya Mungu. Yeye habadiliki, ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye yupo hapa sasa. Mnaamini hilo?

⁷⁵ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Kabla tu hatujaomba, ninyi huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kunaweza kuwako na yeyote hapa, angesema, “Ndugu Branham, nikumbuke, jalia macho yangu ya kiroho yafunguke, nipate kumwona na kumjua Yeye. Jinsi ninavyotaka kumwona! Jinsi ninavyompenda”? Inueni mikono yenu, na kusema, “Nikumbuke.” Mungu awabariki. Bwana abariki, hilo ni jema. Mungu wa Mbinguni na aturehemu. Mtu mwingine huku nyuma upande wangu wa kulia hapa? “Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi.” Mungu awabariki.

⁷⁶ Utajiri usiotafutika wa Kristo, kufunuliwa kwa nguvu Zake na wema Wake! Mungu wa Mbinguni na awape rehema, na fadhili, na neema kwenu nyote.

⁷⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunawaleta wasikilizaji hawa Kwako saa hii, nikiangalia pande zote, nikiona mikono ya watu ikiinuliwa. Mungu asiyebadilika akifanya kazi kwa njia zisizoeleweka, kufanya maajabu Yake! Tunaomba, Ee Mungu, ya kwamba Roho Wako Mtakatifu, Roho Wako atakaa katika kila moyo hapa, usiku wa leo. Wape haja ya mioyo yao. Wafanye wawe na imani, Bwana. Weka kitu ndani yao, ujasiri, wapate kujua ya kwamba Wewe upo daima, u hai daima, kufanya maombezi.

⁷⁸ Umeketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenyezi, na pale kwenye Kiti Chake cha Enzi, mwili wa thamani wa Yesu Kristo umewekwa pale wakati Roho Mtakatifu akiwa duniani, na Yeye yuko pale kama Kuhani wetu Mkuu kutuombea tunapokiri. Kile tunachokiri ya kwamba Yeye atafanya, hicho ndicho Yeye yuko hapo kufanya kiwe sawa. Damu Yake Mwenyewe katika—katika sinia iliyo mbele Zake, mavazi Yake Mwenyewe, yaliyolowa damu, akiketi pale, tukiona kwamba Mungu hawezi kuangalia kupitia kwenye hiyo Damu na kuona udhalimu, kwa sababu Kristo amezichukua dhambi zetu na magonjwa yetu.

⁷⁹ Ee Baba Mungu, tunaomba ya kwamba, Yeye akiwa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, kwamba Yeye ataguswa usiku wa leo na kila udhaifu ulioko jengoni, udhaifu wote, kwamba uwe ni wa kiroho au wa kimwili, kwamba watakuwa na uponyaji, na uamsho utatokea katika mji huu, loo, watu baada ya watu katika Ufalme wa Mungu. Tujalie, Bwana. Sikia maombi yetu.

⁸⁰ Tunakupenda, Baba, nasi tunangojea matarajio makuu Roho Mtakatifu aje miongoni mwetu na kufanya yale aliyoahidi atafanya. Tunaomba hayo kwa ajili yao, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁸¹ Unampenda? Kwa moyo wako wote? Je, unamtazamia Yeye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia? Alisema atafanya mambo makuu mno kuliko yote tuwezayo kufanya au kuwazia. Aliahidi kufanya hivyo.

⁸² Sasa, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye hakudai kuwa mponyaji? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye hakuwa mponyaji? Mnataka kusema hamwijui Biblia vizuri zaidi ya hivyo? Yeye alisema, “Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi.”

⁸³ “Amin, amin, nawaambia,” Yohana 5:19, “amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Hivyo ndivyo alivyosema? Yohana Mtakatifu 5:19, wakati alipojua mahali mtu aliyekuwa hawezi, alipokuwa amelala

kwenye godoro, akamwambia imani yake ingemponya, achukue kitanda chake aende nyumbani.

⁸⁴ Naye alihojiwa miongoni mwa Wayahudi, na akawaacha maelfu ya watu wamelala pale, viwete, vilema, vipofu, waliopindika. Yeye alisema, "Mimi hufanya tu yale Baba anayoniambia, ama, anayonionyesha nifanye. Sasa, ninafanya kile ninachomwona Baba akifanya. Baba anatenda kazi, Nami natenda kazi hata sasa." Sasa, huyo ni Roho Wake.

⁸⁵ Sasa, Yesu Mwenyewe hakufanya uponyaji wowote bila, kwanza, Mungu kumwonyesha, hayo ni Maandiko. "Sifanyi neno isipokuwa Baba anionyeshe kwanza." Sio, "aniambie." "Anionyeshe kwanza." Ndipo anapomwonyesha, Yeye huenda na kufanya yale Baba anayomwambia.

⁸⁶ Yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, sasa, Yeye kamwe hakufanya hivyo, kamwe hakusema alimponya, alisema, "Imani yako imekuokoa. Imani yako imekuokoa."

⁸⁷ Bartimayo kipofu langoni, "Imani yako imekuponya." Hakuwa na uhusiano wowote nalo.

⁸⁸ Imani ya hao watu ilifanya hivyo, kwa sababu waliamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alingusa, yule mwanamke alingusa, naye akagusa vazi Lake. Na sasa, Yeye hakuhisi kimwili, kwa sababu vazi la Kipalestina lina vazi la ndani, nalo joho linapwaya, naye akagusa upindo wake. "Kwa maana alisema moyoni mwake, 'Kama nikigusa tu vazi Lake, nitakuwa mzima.'" Basi akamgusa, na alipomgusa, kwa nini alihisi moyoni mwake, kwa sababu, imani yake ilikuwa, kama angeweza kuligusa, ataponywa, basi akafanya kile alichowazia kwamba kingemletea nguvu za Mungu, naye akahisi kwamba yalitoshia kabisa. Na yalitoshia, kwa sababu aliamini.

Yesu akageuka na kuangalia kote kwenye kusanyiko, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

Petro akamkemea, kasema, "Ati ni nani aliyekugusa? Vema, wote wanakugusa. Kwa nini useme jambo kama hilo?"

⁸⁹ Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu," ama, "nguvu zimenitoka," ambalo linamaanisha *uweza*. "Nimekuwa dhaifu. Mtu fulani alinigusa Mimi kwa mguso wa namna nyingine." Naye akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona huyo mwanamke. Naye akamwambia kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma, kwa sababu imani yake ilikuwa imemponya.

⁹⁰ Sasa, huyo ni Yesu alivyokuwa jana, huyo ni Yesu yeye yule leo, huyo ni Yesu yeye yule Ambaye atakuwako kesho kama kuna kesho, na atakuwako milele.

⁹¹ Wakati watu wanapofikiri ya kwamba Mungu hutoa ahadi wala haitimizi, Waislamu, ama chochote kile... Nimeshika Biblia kwa mkono mmoja na Kurani katika mkono mwingine, na

kusema, “Kimoja ni cha kweli na kingine ni cha uwongo. Vyote viwili haviwezi kuwa vya kweli, maana vinapingana, kimoja kwa kingine.” Ninasema, “Mnathibitisha ya kwamba nabii wenu amekufa, yuko ndani ya mchanga; Yesu wetu alifufuka katika wafu. Naye aliahidi mambo aliyofanya, sisi pia tutayafanya.” Nikasema, “Sasa, hebu niwaone mkifanya kazi za Muhammad. Hamwezi kufanya. Lakini kazi za Yesu Kristo zinafanywa na Roho Mtakatifu, anapokuja kuwatia watu mafuta.”

⁹² Mnaamini hilo? Bila shaka, tunaamini. Ni kitu gani kingetuzuia kuamini? Kwa sababu Mungu alifanya ahadi, Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

⁹³ Sasa, mwanadamu hawezi kufanya hivyo, ni mambo ya kimbinguni, ni jambo ambalo mwanadamu hawezi kufanya. Wakati nikiwa na muda wa dakika chache tu, ninataka kuelezea jambo hilo. Mnaona, mwanadamu hawezi kufanya lolote, ni Mungu ndani ya mwanadamu. Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni tawi.” Sasa, maadamu tawi liko ndani ya Mzabibu, litazaa tunda la Mzabibu. Sasa, Mungu daima aliwatumia wanadamu kama wakala Wake.

⁹⁴ Hiyo ndiyo sababu alimtumia Mwanawe Mwenyewe apate kujifunua. Alishuka na kuchukua mfano wa mwanadamu kusudi afe mauti kwa ajili ya mwanadamu. Asingeweza kufa katika Roho, bali aliuawa katika mwili.

⁹⁵ Basi Mungu alikuwa ndani ya Ibrahimu, Mungu alikuwa ndani ya Isaka, Mungu alikuwa ndani ya Yakobo, Mungu alikuwa ndani ya Yusufu, Mungu alikuwa ndani ya Daudi, Alikuwa katika watu hao wote huko nyuma, hao manabii na kadhalika, ilikuwa ni Mungu akitenda kazi kupitia wanadamu.

⁹⁶ Sasa, katika wakati huu wa Agano Jipya, Damu ya Yesu Kristo hulisafisha Kanisa Lake na kulitakasa, kusudi Roho Wake Mtakatifu aendelee kuiendeleza kazi ya Mungu katika nyakati zote. Naye ni yeye yule leo, kama sivyo, basi sisi ni mashahidi wa uongo wa Biblia hii. Kama hiyo, kama hiyo si kweli, basi Biblia si ya kweli. Wakati umewadia kwa watu kuihubiri Injili, wakati umewadia wa nguvu za Mungu kufanywa zijulikane. Wakati makafiri wakijaribu kulikanyaga Neno hilo, tunahitaji watu kama wale wana wa Kiebrania, “Mungu wetu anaweza kutuokoa na hii.” Hiyo ni kweli. Wakati umewadia. Mungu anabaki yeje yule.

⁹⁷ Sasa, Mungu hawezi kukuponya, kwa sababu tayari amekuponya, wakati, “Alijeruhiwa kwa makosa yako, akachubuliwa kwa maovu yako, adhabu ya amani yako ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake uliponywa.” Ni wakati uliopita.

⁹⁸ Kama angesimama hapa usiku wa leo amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya kama ungemwomba Yeye, angesema, “Tayari nimefanya hivyo, wewe amini.” Huenda

akafanya jambo fulani kukufanya ujue ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Na hivyo ndivyo anavyofanya siku hizi, Yeye hufanya ijulikane kwa watu Wake, kwa watu Wake ya kwamba Yeye ni Mungu, si mwanadamu, bali Mungu.

⁹⁹ Sasa, Yeye ni halisi vivyo hivyo usiku wa leo. Na—najua Yeye yupo hapa. Ni wangapi waliopata kuiona ile picha ya Malaika wa Bwana, ile Nuru? Kuna wengi wenu. Wanayo hapa, nafikiri, mahali fulani. Huenda wale wavulana wanayo, Gene na hao wengine wanayo mezani kule nyuma.

¹⁰⁰ Nuru hiyo, mnakumbuka, mimi, kama sitakutana nanyi tena duniani, nitakutana nanyi Siku hiyo, Nuru hiyo haisimami futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa. Hiyo ni kweli. Aliahidi jambo hilo, nami ninamwamini Mungu. Nimeiona dhidi ya makumi ya maelfu ya makafiri, nimeiona katika nyakati wachawi wakiwa pande zote mbili, na kuona nguvu za Mungu zikiwapoozesha na kuketi pale. Mungu ama ni Mungu, au Yeye si Mungu. Yesu ama ni Mwana wa Mungu, au Yeye alikuwa laghai; Yeye ni Kristo Mwana wa Mungu, Yeye hajafa, bali yu hai, Naye yu hai milele. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁰¹ Ni wangapi wanaamini hilo? Mungu awabariki. Ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Yeye anaweza kutokea moja kwa moja . . . ?

¹⁰² Hatuna kadi za maombi zilizosambazwa, sivyo? Ni wangapi walio wagenjwa huko nje na wanataka uponyaji? Inueni mikono yenu. Semeni, “Mungu, mimi ni mgonjwa, ninahitaji uponyaji.” Inueni tu mikono yenu, mtu yeyote ambaye ni mgonjwa na anataka uponyaji. Inueni tu mikono yenu, na kusema, “Naomba ya kwamba Mungu ataniponya.” Una mpendwa unayemwomba, inua mikono yako, useme, “Ni—ni—ninaomba.” Mungu aturehemu.

¹⁰³ Hakuna mtu katika jengo hili ninayemjua, nje ya, ninaamini, kama sina hakika, huyu ni Pat aliyeketi papa hapa, Pat Tyler. Mimi . . . Sijui kama ninyi nyote mnamjua ama hamumjui. Halafu Ndugu Gene Goad aliyeketi hapa akiurekodi ujumbe.

¹⁰⁴ Watu jukwaani, nilikutana nao jana usiku, kundi la watu wazuri sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu. Lakini wale pekee ninaowajua binafsi ni ndugu papo hapo, alinidhamini mara ya kwanza nilipokuwa hapa, Ndugu Williams, na mwanawe, Ndugu Borders, Ndugu David, na Ndugu Harvey ndio pekee ninaowajua hapa.

¹⁰⁵ Lakini Yesu Kristo anajua kila mmoja wenu kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mwekeni kwenye shindano la kuamua. Yeye ni Mungu? Ni sawa? Yeye anamjua kila mmoja wenu.

¹⁰⁶ Kama Yeye . . . Tunakukaribia kuja kwa Mwana wa Mungu, Yeye alijithibitishaje Mwenyewe kuwa ni Mungu, na kuwa Mwana wa Mungu kwa Wayahudi? Wakati alipomtambua Petro

kwamba yeye alikuwa ni nani; alisema, alimwambia Nathanaeli mahali alipokuwa wakati alipokuwa chini ya mtini, alipomwona chini ya mti, akiomba. Akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi kwa mataifa ya Wayahudi.

107 Kasisi akarudi, akasema, “Yeye ni mpiga ramli.”

108 Naye akasema, “Ukisema hivyo kunihusu Mimi, nitakusamehe, lakini ajapo Roho Mtakatifu, afadhali usiongee dhidi Yake basi, kwa sababu halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Angalia kwamba . . .

109 Vema, kuna matabaka matatu tu ya watu, hao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, hao ni Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria. Mnamkumbuka Petro wakati wa Pentekoste? Aliwahubiria Wayahudi, akafungua Ufalme; kwa Wasamaria wakati Filipo alipokuwa ameshuka na kuwabatiza, walakini hawakumpokea Roho Mtakatifu; huko chini nyumbani kwa Kornelio, basi wote walikuwa wamemsikia: Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Roho Mtakatifu wakati huo alikuwa . . . Hawakumhitaji tena kwa kusudi hilo, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa amewaendea watu wote.

110 Wakati Yesu alipokuja, sisi Wamataifa tulikuwa Waanglo-Sakson ambao hatukumtazamia Masihi ajaye, tulikuwa makafiri na marungu mgongoni mwetu. Lakini hao waliokuwa wakimtazamia Masihi, kulikuwako na Wayahudi na Wasamaria wakimtazamia Masihi . . . Wakati alipotokea, vipi, alifanya ishara ya namna gani? Alifanya ishara ya Nabii ambaye Musa alinena habari Zake, angekuwa ni Mungu-Nabii. Wakaliangalia, wale ambao kweli wanaongozwa kiroho, walimwona akifanya ishara hiyo, nao wakasema, “Huyo Ndiye!”

111 Lakini wale wengine waliokuwa na mafunzo yao yote ya kiakili, walisema, “Jamaa huyu ni Beelzebuli.”

112 Alienda huko Samaria, alikuwa na haja. Mwanamke alikuja kisimani, Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.”

Naye mwanamke anasema, “Si kawaida, tuna ubaguzi hapa. Wayahudi na Wasamaria hawana uhusiano.”

Akasema, “Mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

Akasema, “Kisima ni kirefu, Nawe una . . .”

113 Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiwasiliana na roho yake. Ndipo alipoona shida yake ilipokuwa, sote tunajua ilikuwa ni nini, ambapo shida yake ilikuwa, Yeye alisema, “Nenda, kamwite mumeo, mje hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

Kasema, “Ulisema kweli, una watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

¹¹⁴ Akasema, ati “Bwana, naona kwamba wewe ni Beelzebuli”? La bwana. Alisema, “Naona kwamba Wewe ni nabii. Naona kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua, tunajua, sisi Wasamaria, tumefundishwa, tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya.” Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. “Lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Loo, jamani!

¹¹⁵ Kumbukeni, Yeye kamwe hakufanya hivyo kwa Mataifa, hakufanya hivyo kwa Mataifa. Basi kama Yeye ni Mungu asiye na kikomo, kisha anawaacha, wakiwa na mafundisho ya kiakili kadiri tulivyo nayo siku hizi, kama tukiingia kwenye. . . kutoka kwenye hiki, kipindi chetu cha wakati, bila dhihirisho lile lile, basi Yeye aliwafanyia jambo ambalo hakutufanyia sisi. Lakini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Aliahidi angefanya hivyo.

¹¹⁶ Alifanya nini? Maandiko mengi, bali lile ambalo ndiyo kwanza ninukuu, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Ndivyo itakavyokuwa, jambo lile lile litatukia kabla tu ya ule Moto. Huyu hapo, Mungu asiye na kikomo; Yuko hapa usiku wa leo. Hilo ni jambo kubwa la kusema, bali ni jambo ambalo Biblia ilisema hivyo, naye Roho Mtakatifu yuko hapa kuliunga mkono na kusema ni kweli. Hiyo ni kweli, ndugu.

Na tuombe.

¹¹⁷ Ee Bwana, kuna mtu hapo anayeteseka, hapana shaka, watu fulani wana haja. Ninakuomba Wewe, Baba, uturehemu na ujalie tu ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu. Sema tu Maneno, Bwana, nami naomba ya kwamba maskini mtu fulani hapa ndani, anayekutafuta Wewe, kwamba wataweza kungusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Lijalie tu, Bwana, angalau mmoja au wawili, ili watu wapate kujua kwa kinywa cha shahidi mmoja au wawili, au, mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitishwe. Tujalie, Baba.

¹¹⁸ Niliomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kwa ajili ya ujumbe usiku wa leo, Bwana, na Neno Lako linalotangaza kwamba ndivyo ilivyo, ili watu wapate kujua ya kwamba wakati wa kufunuliwa na kuwekwa wazi umewadia, kwamba Wewe uko hapa yule yule jana, leo, na hata milele. Amina.

¹¹⁹ Sasa ninawatakeni muombe. Nataka uamini kwa moyo wako wote na yote yaliyo ndani yako kuamini ya kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu yupo hapa.

¹²⁰ Ni wangapi ambao siwajui huko nje, ambao siwajui? Inueni mikono yenu. Kote kote jengoni, haijalishi uko wapi. Sasa, labda hujawahi kujua jambo hili. Sasa, kama . . .

¹²¹ Itanibidi kumfuata Roho Mtakatifu, na kama akinena, wewe jibu. Sisemi ya kwamba atanena, ninasema tu naomba ya

kwamba atanena, mnaona, kwamba atanena. Sina haki ya kusema hivyo, ila tu kwa Neno Lake, Yeye alisema ya kwamba atalijalia, nasi tunaamini ya kwamba litajaliwa.

¹²² Sasa ninyi ombeni. Sasa ni imani yenu, huwezi kufanya lolote mpaka umguse Yeye, ndipo Yeye anene nami. “Kama unaweza kuamini! Kama unaweza kuamini!”

¹²³ Naam, hii hapa. Hebu kidogo. Papa hapa mkono wangu wa kushoto, huyo hapo mwanamke ameketi hapo, kidogo ni mnene. Yeye ni mahututi kabisa, ana ugonjwa wa moyo, ametiwa uvuli na kansa, kiroho, mfadhaiko wa pepo, ukandamizaji, hasa. Huyu mama huketi papa hapa ameinamisha kichwa chake, akiniangalia moja kwa moja huku. Unaamini, mama, ya kwamba Yesu Kristo atakuponya? Unaamini? Unaamini? Unaukubali? Umeipoteza.

¹²⁴ Sasa, itakubidi kushinda hilo. Hmm!

¹²⁵ Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, acha ijulikane, ili watu wapate kufahamu, Bwana.

¹²⁶ Mwaminini Mungu.

¹²⁷ Huyu hapa mwanamume ameketi papa hapa nyuma, akimwombea mkewe, anawaza juu ya mkewe, anamwombea. Amefanyiwa upasuaji na kadhalika, wala hauonekani kumsaidia hata kidogo. Hiyo ni kweli kabisa. Mtu huyo ni mhudumu, Kasisi Nathan, Jacob Nathan, mke wako ameketi karibu nawe, unaamini ya kwamba Yesu Kristo atamponya? Unaukubali, bwana? Inua mkono wako kama unaukubali. Mungu akubariki, endelea.

¹²⁸ Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu. Mwamini Mungu. Usiache hilo likupite. Yeye ni Mungu milele.

¹²⁹ Huyu hapa mwanamke ameketi, aliinamisha kichwa chake papo hapo, ameketi hapo, akiniangalia sasa. Mwanamke huyo ni mlemavu, kwa namna fulani, ana mkongojo chini yake anaotembelea. Unaamini, mama, ya kwamba Yesu Kristo atakuruhusu utoke hapa bila hiyo mikongojo usiku wa leo? Unaamini, uliyeketi moja kwa moja hapo ukiniangalia? Je, utaukubali, uponyaji wako? Inua mikono yako. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini kama utaamini, utaiacha imewekwa hapo, kisha utoke nje, na uwe mzima.

¹³⁰ Ninaipa changamoto imani yako kuamini! “Kama unaweza kuamini!”

¹³¹ Vipi kuhusu hapa nyuma sasa? Vipi kuhusu ninyi wahudumu? Ninyi ndugu mnaamini? Kwa moyo wenu wote? Sasa, hatufahamiani, mbali na Ndugu Williams. Mungu anawapenda, ninyi ni watumishi Wake, nipo hapa kuwa ndugu yenu. Roho wa Mungu yupo hapa, nasema hilo kwa ujasiri katika Jina la Yesu Kristo. Iweni tu na imani na muamini. Kama kuna shida, mwulizeni Yeye.

¹³² Mtu huyu aliyeketi papa hapa akiniangalia, si wewe hasa, ni baba yako aliyeketi huko nje. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia ana shida gani? Ungeamini? Katika miguu yake, hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Huyu hapo baba yake ameketi papo hapo, mzee, kidogo mwenye upara, ameketi hapo, akiniangalia moja kwa moja sasa.

¹³³ Hapa, angalieni hapa, hivi hamwoni hiyo Nuru? Angalieni hiyo Nuru juu ya maskini mwanamke huyu hapa. Anaomba, pia, anamjua mwanamke huyo aliyeketi papo hapo, maskini mwanamke huyo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake? Utaamini? Iko kwenye miguu yake. Hiyo ni kweli.

¹³⁴ Unamwamini Mungu? Unaamini kwamba Malaika wa Bwana, Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele? Yeye anabaki Mungu, wala hakuna kitu kinachoweza kudhuru, hakuna kinachoweza kuzuia. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anaishi milele, yu hai daima kufanya maombezi. Kama tutaamini tu, aminini, Mungu atatimiza yaliyosalia. Unaamini hayo kwa moyo wako wote?

¹³⁵ Sasa, mnaamini ya kwamba kuja kwa Masihi kumekaribia. Watu hao ni nini? Sijawahi kumwona mmoja wao maishani mwangu, naye Mungu anajua hilo kuwa ni kweli.

¹³⁶ Sasa mmeifanya ianze kazi, sasa inazunguka tu kote jengoni. Sasa hivi ndio wakati... Sasa huu ndio wakati wa kupokea uponyaji wenu. Wekeeni mikono yenu mmoja juu ya mwenzake, wekeaneni mikono, na muamini sasa. Sasa mmeupata, sasa mna—mnaingia katika imani.

¹³⁷ Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, na ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Umeifanya ijulikane, Wewe ni Mungu. Na jalia Roho Wako Mtakatifu ashuke katika hili, miongoni mwa watu hawa, na kuwathibitishia ya kwamba Wewe ni Yehova Mungu Mkuu, ya kwamba Wewe unabaki yeye yule jana.

¹³⁸ Shetani, umeshindwa. Toka ndani ya watu hawa, nakuapisha kwa nguvu za Mungu aliye hai, kwamba utoke ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu!

¹³⁹ Vema, ndugu. 

60-0326 Mungu Asiyebadilika
Municipal Auditorium
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org